**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI RUANGWA.

**Juni, 2023**

**RUANGWA- LINDI**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**MAWASILIANO.**

**Mkuu wa Shule:0769 323079**

**Makamu Mkuu wa Shule0786 240629**

**Patron 0786 240629**

**Shule ya Sekondari  Ruangwa**

**S.L.P.47**

**10/06/2023**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………...........................**
**S.L.P ……………………………………..**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI RUANGWA HALMASHAURI YA WILAYA YA RUANGWA MKOA  WA LINDI MWAKA 2023.**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka  2023 na atasoma tahasusi ya ………….

Shule ya Sekondari Ruangwa umbali wa Kilometa 1.5 Mashariki mwa Mji wa Ruangwa Usafiri unapatikana katika kituo cha mabasi nauli ni Shilingi 2000/= kwa pikipiki na Shilingi 3000/= kwa bajaji.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe 14/08/2023 hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 13/08/2023 Mwisho wa kuripoti ni tarehe 31/08/2023.

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**2.1 Sare za Shule**

i. Sare ya shule hii ni light blue kwa Wavulana
ii. Mashati 02 meupe mikono mirefu
iii. Sare ya Michezo ni bukta moja, t-shirt ya blue, track suit ya blue na viatu vya michezo kwa wavulana
iv. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;
v. Soksi jozi mbili nyeusi
vi. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali;
vii. Sweta 1 ya light blue iwe ya kufuma.
viii. Nguo za kushindia (*shamba dress*) suruali nyeusi mbili na T-shirt 2 za blue zisiyo na maandishi
ix. Tai 2 za rangi ya light blue.

**2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo:-**

i. Madaftari 12 counter book
ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika
iv. Scientific Calculator;
v. Godoro la sponji $2^1/_2$ x 6
vi. Mashuka Jozi 2, rangi ya blue, foronya ya godoro 1, chandarua 1 rangi ya blue.
vii. Nguo za ndani za kutosha;
viii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
ix. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
x. Kwanja 1, jembe 1, reki 1, mifagio 2 wa ndani na nje.

**2.3 Michango mbalimbali**

Mzazi au mlezi unapaswa kuchangia michango ifuatayo kupitia akaunti ya shule **Na. 71101100094 NMB** Jina la akaunti **: Ruangwa Secondary School Recurrent Account**).

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku (Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari;
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**
- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**
- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2. Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi au wanajamii;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kusababisha mimba;
xii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xiv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xv. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvi. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xvii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**Karibu Sana Katika Shule Hii**
**Saini ya Mkuu wa Shule:**
**Jina la Mkuu wa Shule . GILBERT M. ASSEY**
**Mhuri wa Mkuu wa Shule :**

HEAD OF SCHOOL
RUANGWA SECONDARY SCHOOL
P. O. BOX 47
RUANGWA

**NB:** Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa**.**

**TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- ➢ **Mkuu wa shule : O769 323079/0710 401 999**
- ➢ **Makamu Mkuu wa Shule:0786 240629**
- ➢ **Mwandamizi Taaluma: 0733 551436**
- ➢ **Mwandamizi Malezi:0786 953868**

**RUANGWA DISTRICT COUCIL**

RUANGWA SECONDARY SCHOOL,

**REF. No………………………………**

**THE MEDICAL OFFICER……………………………………**

**RE: REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION OF ………………………………………**

Please Examine the above-named pupil and give us a regarding his/her suitability for Secondary School studies.

1. Pupil's full name

…………………………………………………..……………………………….

2. Blood.......................................................................................................

3. Stool...............................................................................................................

4. T.B test..........................................................................................................

5. Syphilis test...................................................................................…......

6. Urine examination ……………………………………………………………..

7. Eye test.......................................................................................................

8. Chest...........................................................................................................…...

9. Ear...............................................................................................................

10. Spleen.........................................................................................................

11. Abdomen test.............................................................................................…..

12. Pregnant test (girls only) …………………………..………………………

I certify that the above pupil is suitable/for studies

If unsuitable please give reasons.........................................................................

**………………………………………………………………………………………….**

Name of MEDICAL Officer.......................................................................

Signature of Medical Officer …………………………

Date......................................................................

Official Stamp.........................................................................

**HALMASHAURI YA WILAYA YA RUANGWA**

**SHULE YA SEKONDARI RUANGWA**

**FOMU YA KUJIANDIKISHWA SHULENI NA TAARIFA ZA MZAZI NA MWANAFUNZI.**

**SEHEMU A: TAARIFA ZA MWANAFUNZI**

1. Jina kamili (kama kwenye mtihani wa kumaliza elimu ya msingi) ……………………………………………………

2. Tarehe ya kuzaliwa ……………………………………………………………………….

3. Kabila …………………………………………………………………………………….

4. Mahali na Wilaya alipozaliwa ………………………………………………………….

5. Shule alipomaliza Darasa la Saba ……………… …………………………………………

6. Kidato anachokuja kuingia ……………………………………………………………….

7. Michezo anayopendeleya

| | |
|---|---|
| 1 | |
| 2 | |
| 3 | |

**UONGOZI WA SHULE**

Kazi yoyote ya uongozi aliyowahi kufanya kama vile. Kiranja, Kiongozi wa Kwaya, Ngoma Michezo n.k.

| S/N | NAFASI YA UONGOZI | SHULE | MWAKA |
|---|---|---|---|
| 1 | | | |
| 2 | | | |
| 3 | | | |

Nathibitisha kwamba habari zilizotolewa hapo juu ni kamili na za ukweli

**Tarehe ……………………………** **saini…………………………………………**

## SEHEMU B: TAARIFA ZA MZAZI/MLEZI

i. Jina kamili..........................................................................................................

ii. Kazi..........................................................................................................

iii. Nyumbani..........................................................................................................

iv. Kata..........................................................................................................

v. Tarafa..........................................................................................................

vi. Anwani ya Mzazi/Mlezi ……………………………………………………………….

vii. Namba ya simu ……………………………………………………………………

viii. Dini ………………………………………………………………………………………

ix. Anuani kamili ya nyumbani ambako mtoto atakuwa anakwenda siku za likizo……………………

Ninaahidi kushirikiana na Walimu ili kuhakikisha kwamba kijana wangu anakuwa na tabia nzuri, mchapakazi na mwenye bidii ya kusoma.

Mimi ………………………………………………………………………………………….

Mzazi/Mlezi ninathibitisha kuwa taarifa hiyo hapo juu ni sahihi

Tarehe ………………………………………… saini……………………………………

## MKATABA WA MWANAFUNZI KUHUSU KUTOSHIRIKI KATIKA MIGOMO, FUJO NA MAKOSA YA JINAI

Mimi ………………………………………………………..nimeyasoma kwa makini maelezo haya ya kujiunga na shule. Kwa hiari yangu nakubaliana nayo.

Naahidi nitaheshimu sheria, kanuni na taratibu zote za shule na miongozo mbalimbali itakayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini. Aidha naahidi kuwa kwa vyovyote vile sitashiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai nikiwa shuleni au nje ya shule.

Endapo nitavunja sheria, kanuni, taratibu za shule, kushiriki katika migomo, fujo na kutenda makosa ya jinai, basi nichukuliwe hatua stahiki kulingana na kosa nitakalokuwa nimefanya.

Saini ya Mwanafunzi..........................................................................................

Saini ya Mzazi......................... .................................................

Saini ya Mkuu wa shule:



